JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**WIZARA YA KILIMO**

## BODI YA KOROSHO TANZANIA

# MWONGOZO NA.3 WA UNUNUZI WA KOROSHO KWENYE SOKO LA AWALI KWA AJILI YA WABANGUAJI WA NDANI KWA MSIMU WA 2025/2026

**TOLEO LA TANO**

28th August, 2025.


Mkurugenzi Mkuu

Bodi ya Korosho Tanzania (CBT)

74 Barabara ya Tanu

S. L. P 533

**63104 MTWARA**

**YALIYOMO** **UKURASA**


1.0. UTANGULIZI ..... 1

2.0. MADHUMUNI YA MWONGOZO ..... 1

3.0. UTARATIBU WA UNUNUZI WA KOROSHO KATIKA SOKO LA AWALI ..... 1

3.1. Upatikanaji wa Leseni ya Ununuzi wa Korosho ..... 2

3.2. Utaratibu wa Ununuzi wa Korosho Ghafi katika Soko la Awali ..... 2

3.3. Uhakiki na Udhibiti wa Ubora wa Korosho katika Soko la Awali ..... 3

3.4. Utaratibu wa Malipo ..... 3

3.5. Usafirishaji ..... 4

3.6. Utoaji wa taarifa ..... 5

4.0. MGAWANYO WA MAJUKUMU ..... 6

4.1. Wizara ya Kilimo ..... 6

4.2. Wizara ya Viwanda na Biashara ..... 6

4.3. Bodi ya Korosho Tanzania ..... 6

4.4. Sekretarieti za Mikoa ..... 7

4.5. Ofisi za Wakuu wa Wilaya ..... 7

4.6. Halmashauri za Wilaya ..... 7

4.7. Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania ..... 8

4.8. Chama Kikuu cha Ushirika (*Union*) ..... 8

4.9. Chama cha Ushirika cha Msingi (AMCOS) ..... 8

4.10. Mbanguaji wa ndani ..... 9

4.11. Umoja wa Wabanguaji wa Korosho nchini TACP ..... 9

4.12. Mkulima wa Korosho ..... 10

4.13. Taasisi za Fedha ..... 10

5.0 MAKOSA NA ADHABU ..... 11

6.0 USULUHISHI WA MIGOGORO ..... 11

7.0 HITIMISHO ..... 12

## TASFIRI YA MANENO

Katika mwongozo huu, maneno yafuatayo yanatafsiriwa kama ifuatavyo: -

| | |
|---|---|
| ***AMCOS*** | *(Agricultural and Marketing Cooperative Societies)* Ni Chama cha Ushirika cha Msingi kilichoundwa na Wanachama kwa mujibu wa Sheria namba 6 ya Vyama vya Ushirika ya Mwaka 2013. |
| ***CBT*** | *(Cashewnut Board of Tanzania)* Bodi ya Korosho Tanzania |
| ***Chama Kikuu (Union)*** | Chama Kikuu cha Ushirika kilichoundwa na muunganiko wa vyama vya ushirika vya msingi kwa mujibu wa Sheria namba 6 ya Vyama vya Ushirika ya Mwaka 2013. |
| ***Mhakiki wa Ubora*** | Mtaalamu aliyefuzu mafunzo ya uhakiki ubora wa Korosho na kupata cheti cha uhakiki kutoka Bodi ya Korosho Tanzania na kuajiriwa na mtunza ghala kwa ajili ya kuhakiki ubora wa Korosho zinazoingizwa kwenye ghala la mnada. |
| ***Mkulima*** | Mtu yeyote anayelima zao la korosho |
| ***Mnunuzi*** | Mfanyabiashara aliyesajiliwa na TACP, mwenye kiwanda nchini na ana leseni ya ununuzi wa Korosho katika Soko la Awali kutoka Bodi ya Korosho Tanzania katika msimu husika. |
| ***Msafirishaji*** | Msafirishaji wa Korosho kutoka ghala la AMCOS kwenda ghala la mnunuzi/kiwandani. |
| ***Mbanguaji*** | Kampuni/Mtu binafsi mwenye leseni ya Ubanguaji wa Korosho nchini Tanzania. |
| ***PDN*** | (*Produce Dispatch Note*) ni hati ya kusafirisha Korosho kutoka eneo moja kwenda lingine ndani ya nchi. |
| ***Sheria*** | Sheria ya Tasnia ya Korosho Na.18 ya Mwaka 2009 na Kanuni |

zake za mwaka 2010, Sheria ya Stakabadhi za Ghala ya Sura 339 *R.E.* ya Mwaka 2016 na Kanuni zake za Mwaka 2016, na Sheria ya Vyama vya Ushirika Na.6 ya Mwaka 2013 pamoja na Kanuni zake 2015 pamoja na Kanuni, miongozo na taratibu zinazoweza kuandaliwa chini ya Sheria husika.

**TACP** — Tanzania Association of Cashewnut Processors (Umoja Wabanguaji wa Korosho Tanzania)

***TCDC*** — *(Tanzania Cooperative Development Commision)* Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania

***Tozo*** — Ni gharama atakazotozwa mnunuzi wakati wa mauzo ya korosho ambazo zimekubalika katika mkutano mkuu wa wadau wa korosho nchini.

***Soko la Awali*** — Ni mfumo wa mauzo ambao mbanguaji wa ndani na mkulima watafanya mauziano ya korosho ghafi kupitia AMCOS.

**Leseni** — Kibali kinachotolewa na Bodi ya Korosho kupitia mfumo wa kieletroniki wa Wizara ya Kilimo (e-kilimo) chenye kumruhusu mtu au kampuni kununua korosho ghafi kupitia mfumo wa Soko la Awali.

## 1.0. UTANGULIZI

Serikali imeweka lengo la kubangua asilimia 100 ya korosho zitakazokuwa zinazalishwa hapa nchini ifikapo 2030 ili kuongeza mchango wa zao la korosho katika kufikia ajenda 10/30. Ubanguaji wa korosho hapa nchini utasaidia nchi kunufaika zaidi na zao la korosho kwa kuuza korosho iliyoongezwa thamani. Aidha, ongezeko la ubanguaji litasaidia kupanua wigo wa soko la korosho zinazozalishwa hapa nchini pamoja na kuchagiza uzalishaji wa bidhaa zingine zinazotokana na korosho. Pia, ubanguaji wa korosho una mchango mkubwa katika kuongeza ajira hususani kwa wanawake na vijana.

Ili kufikia lengo hilo, mikakati mbalimbali imewekwa ili kuhamasisha ubanguaji wa korosho hapa nchini. Miongoni mwa mikakati hiyo ni kuanzishwa kwa soko la awali ili kuwawezesha wabanguaji wa ndani kununua korosho bila kushindana na wasafirishaji wa korosho ghafi nje ya nchi (Exporters). Hatua hii ya Serikali inalenga kuwawezesha wabanguaji wa ndani ya nchi kuweza kupata malighafi (korosho) za kutosheleza mahitaji ya viwanda vyao. Kwa mujibu wa Mwongozo huu wabanguaji wa ndani wenye viwanda vilivyopewa Leseni na Bodi ya Korosho na ambao ni wanachama wa Tanzania Association for Cashewnut Processors (TACP) ndio watakaoruhusiwa kununua korosho ghafi katika Soko la Awali kwa kiasi cha kutosheleza mahitaji yao ya msimu husika.

## 2.0. MADHUMUNI YA MWONGOZO

Madhumuni ya Mwongozo huu ni kuweka utaratibu utakaowawezesha wabanguaji wa ndani kununua korosho kwa ajili kubangua katika viwanda vya ndani. Pia, masharti ya mwongozo yamelenga kuhakikisha kuwa korosho zote zitakazonunuliwa katika mfumo wa soko la awali zinabanguliwa nchini.

## 3.0. UTARATIBU WA UNUNUZI WA KOROSHO KATIKA SOKO LA AWALI

Utaratibu wa ununuzi wa korosho ghafi katika Soko la Awali unahusisha upatikanaji wa vibali vya ununuzi, mfumo wa uuzaji, udhibiti wa ubora wa korosho, utaratibu wa malipo, usafirishaji na utoaji wa taarifa.

### 3.1. Upatikanaji wa Leseni ya Ununuzi wa Korosho

i. Mbanguaji ataomba leseni ya kubangua korosho nchini kwa kutuma barua ya maombi Bodi ya Korosho.

ii. Bodi ya Korosho itafanya ukaguzi wa kiwanda na kutoa leseni ya ubanguaji.

iii. Mbanguaji atajisajili TACP na kupewa barua ya utambulisho.

iv. Mbanguaji atasaini Mkataba wa ununuzi wa korosho ghafi kutoka Soko la Awali na kubangua nchini.

v. Mbanguaji ataomba leseni ya kununua korosho katika Soko la Awali kwa ajili ya kubangua ndani ya nchi kupitia mfumo wa kieletroniki ulioko chini ya Wizara ya Kilimo ***'eKilimo' (https://ekilimo.kilimo.go.tz)*** akiainisha mahitaji ya korosho ghafi na uwezo wa kiwanda kubangua korosho hizo.

vi. Bodi ya Korosho itafanya tathmini ya maombi na kumpatia leseni.

vii. Bodi ya Korosho itaandika barua kwenda Ofisi ya Mkuu wa Mkoa kwa ajili ya kuwatambulisha wabanguaji waliopata leseni ya kununua korosho Soko la Awali na watakaonunua kwenye mkoa husika.

### 3.2. Utaratibu wa Ununuzi wa Korosho Ghafi katika Soko la Awali

i. Ununuzi wa korosho ghafi katika Soko la Awali (*Primary Market*) utaanza tarehe 1 Septemba, 2025 hadi 31 Agosti 2026.

ii. AMCOS zote zitaruhusiwa kuuza korosho ghafi kupitia Soko la Awali chini ya usimamizi wa Chama Kikuu.

iii. Chama/Vyama vya Msingi (AMCOS) vyenye korosho za wakulima ambao wameridhia kuuza kupitia soko la awali vitatoa taarifa kwa Chama Kikuu husika juu ya kiasi cha korosho kilichopo kwa ajili ya kukamilisha taratibu za manunuzi.

iv. Kabla ya mauziano Mnunuzi na Mtaalam wa ubora kutoka Bodi ya Korosho au Halmashauri au Chama Kikuu watahakiki ubora na kiasi cha korosho katika ghala husika.

v. Wakulima watakuwa na hiari ya kuuza korosho ghafi katika Soko la Awali

au Soko la Upili.

vi. Bei ya korosho ghafi katika Soko la Awali ni ile itakayokubalika baada ya mapatano ya bei kati ya Mkulima na Mbanguaji.

vii. Mbanguaji atatakiwa kulipia korosho pamoja na ushuru wa Halmashauri (*Crop Cess*), ushuru wa Union, ushuru wa AMCOS, tozo ya usimamizi na utafiti pamoja na gharama/tozo nyingine kama zitakazokuwa zimeidhinishwa na mkutano mkuu wa wadau wa korosho. Tozo zote zitalipwa kabla ya mbanguaji kutoa korosho kwenye ghala la AMCOS.

viii. Tozo zote zilizotajwa katika kifungu 3.2 (vii) zitalipwa Chama Kikuu cha Ushirika, Aidha Tozo ya usimamizi na utafiti zitalipwa Bodi ya korosho kupitia Akaunti Namba itakayoainishwa.

ix. Mbanguaji atawajibika kutumia magunia yenye nembo ya kiwanda chake wakati wa kutoa korosho alizonunua kutoka ghala la AMCOS kwenda kiwandani.

x. Mbanguaji atatakiwa kubangua hapa nchini korosho zote atakazonunua kupitia kwenye mfumo wa Soko la Awali. Kwa sababu yoyote ile korosho zitakazonunuliwa katika mfumo wa Soko la Awali hazitaruhusiwa kusafirishwa nje ya nchi zikiwa ghafi.

xi. Mbanguaji haruhusiwi kufunga mkataba au kufanya biashara ya mauziano ya korosho na vikundi ambavyo sio AMCOS. Badala yake Mbanguaji atapaswa kununua au kufunga mkataba wa kununua korosho kwenye vyama vya msingi (AMCOS) chini ya usimamizi wa vyama vikuu.

## 3.3. Uhakiki na Udhibiti wa Ubora wa Korosho katika Soko la Awali

Uhakiki wa ubora wa korosho ghafi katika Soko la Awali utazingatia Mwongozo wa Usimamizi wa Ubora wa Korosho uliotolewa na Bodi ya Korosho katika msimu wa mwaka 2025/2026.

## 3.4. Utaratibu wa Malipo

i. Mbanguaji atatakiwa kulipia korosho alizonunua moja kwa moja kwenye akaunti ya Mkulima chini ya usimamizi wa Chama cha Msingi (AMCOS) na Chama Kikuu husika. Malipo kwa mkulima hayatahusisha tozo au

gharama zingine zilizoainishwa katika kipengele namba 3.2(vii).Tozo zingine zitalipwa katika akaunti za wadau husika kwa utaratibu utakaoainishwa katika mkataba wa kununua korosho katika Soko la Awali.

ii. Malipo yafanyike ndani ya siku mbili (2) baada ya kukamilika taratibu za mauziano, na iwapo mnunuzi atashindwa kulipa atatozwa faini ya asilimia 5% ya thamani ya mzigo aliounununua. Aidha mkulima mwenye korosho hizo atakuwa na hiari kuziuza kwa mnunuzi mwingine soko la awali au kuuza kupitia soko la upili. Faini ya 5% italipwa Bodi ya Korosho Tanzania kupitia nambari ya utambuzi wa malipo "Control Number",aidha kwa sababu zozote zile mnunuzi hataruhusiwa kusafirisha mzigo kutoka katika ghala la Chama cha Msingi (AMCOS) iwapo atakuwa hajakamilisha malipo kwa wakulima na tozo nyingine kama zilivyoainishwa katika kipengele namba 3.2(vii) cha mwongozo huu.

iii. Mbanguaji hataruhusiwa kuchukuwa korosho ghafi za wakulima hadi atakapo kamilisha malipo ya korosho zote alizonunua pamoja na tozo.

### 3.5. Usafirishaji

i. Mbanguaji atatakiwa kuomba idhini ya kusafirisha korosho ghafi alizozinunua katika Soko la Awali kutoka kwa Halmashauri akiwa ameambatisha nyaraka zinazothibitisha ukamilifu wa malipo ya korosho husika. Idhini toka Halmashauri itatolewa baada ya malipo ya mkulima pamoja na tozo zote kukamilika.

ii. Bodi ya Korosho itatoa kibali (PDN) cha usafirishaji wa korosho ndani ya nchi baada ya kupokea idhini iliyotolewa na Halmashauri aliyonunua korosho kupitia soko la awali.

iii. Mbanguaji atatakiwa kuzingatia taratibu nyingine zote za usafirishaji wa korosho kama zilivyoainishwa katika Mwongozo namba moja (1) wa Usimamizi wa Masoko uliotolewa na Bodi ya Korosho kwa msimu wa 2025/2026.

### 3.6. Utoaji wa taarifa

Bodi itapata taarifa ya kiasi cha korosho ghafi kilichonunuliwa na mbanguaji katika halmashauri husika kila wiki kutoka Chama Kikuu husika. Hata hivyo, Mbanguaji anawajibika kutoa taarifa ya ununuzi wa korosho ghafi katika Soko la Awali na korosho zilizobanguliwa Bodi ya Korosho Tanzania kila wiki.

## 4.0. MGAWANYO WA MAJUKUMU

Ili kuhakikisha kuwa changamoto za uhaba wa malighafi kwa wabanguaji wa ndani zinapatiwa ufumbuzi, majukumu ya kiutendaji na kitaasisi yamegawanywa katika makundi mbalimbali ya wadau kama ilivyoelezwa hapa chini.

### 4.1. Wizara ya Kilimo

i. Kutoa na kusimamia miongozo ya kisera juu ya upatikanaji wa korosho kwa viwanda vya ndani.

ii. Kuunganisha wadau wa Tasnia ya Korosho nchini katika kufikia malengo ya kuongeza thamani na masoko ya korosho inayozalishwa nchini.

iii. Kuelekeza na kuweka mfumo wa upatikanaji wa mitaji kwa wabanguaji wa ndani kupitia Bodi ya Korosho kwa kushirikiana na wadau wengine Pamoja na taasisi za fedha.

iv. Kusimamia utekelezaji wa Mwongozo huu ndani ya Mkoa husika.

### 4.2. Wizara ya Viwanda na Biashara

i. Kutoa na kusimamia miongozo ya kisera juu ya uanzishwaji na uendelezaji wa viwanda vya kubangua korosho nchini; na

ii. Kuunganisha jitihada za wabanguaji katika kutafuta masoko ya korosho iliyobanguliwa pamoja na bidhaa zake.

iii. Kusimamia utekelezaji wa Mwongozo huu.

### 4.3. Bodi ya Korosho Tanzania

i. Kupokea maombi ya mahitaji ya korosho ghafi kwa wabanguaji wa *ndani* kwa kushirikiana na Umoja wa Wabanguaji Korosho nchini.

ii. Kuandaa mkataba wa makubaliano ya ununuzi wa korosho katika soko la awali kati ya Bodi ya korosho TACP na mbanguaji.

iii. Kutoa leseni ya ubanguaji wa korosho kwa wamiliki wa viwanda nchini.

iv. Kutoa leseni ya ununuzi wa korosho ghafi kupitia mfumo wa Soko la Awali.

v. Kusimamia uendeshaji wa Soko la Awali.

vi. Kutoa elimu kwa wakulima juu ya gharama za uzalishaji wa korosho

ghafi ikiwa ni pamoja na faida kwa mkulima/wakulima husika ili wawe na uelewa wa kutosha wakati wa kufanya mapatano ya bei ya kununulia korosho kutokakwenye Soko la Awali.

vii. Kufanya ufuatiliaji na tathmini ya zoezi la ununuzi wa korosho ghafi katika Soko la Awali.
viii. Kuwatambulisha wabanguaji katika Sekretarieti za Mikoa na Vyama Vikuu vya Ushirika.
ix. Kutatua changamoto zozote zitakazojitokeza katika utekelezaji wa Soko la Awali.
x. Kuchukua hatua za kisheria kwa wadau watakaokiuka Mwongozo huu.
xi. Kusimamia utekelezaji wa Mwongozo huu.

### 4.4. Sekretarieti za Mikoa

i. Kuwatambulisha wabanguaji walioidhinishwa na Bodi ya Korosho kwa Halmashauri husika kwa ajili ya ununuzi wa korosho katika Soko la Awali.
ii. Kusimamia utekelezaji wa Mwongozo huu ndani ya Mkoa husika.

### 4.5. Ofisi za Wakuu wa Wilaya

Kusimamia utekelezaji wa Mwongozo huu ndani ya wilaya husika.

### 4.6. Halmashauri za Wilaya

i. Kuwatambulisha wabanguaji walioidhinishwa na Bodi ya korosho kwa Chama Kikuu cha Ushirika (UNION) na Vyama vya Msingi (AMCOS) kwa ajili ya ununuzi wa korosho katika soko la awali.
ii. Kutoa idhini ya usafirishaji wa korosho ghafi ndani ya halmashauri baada ya kupata uthibitisho wa malipo ya korosho alizonunua kutoka AMCOS husika.
iii. Kuwasimamia Maafisa Ushirika katika utekelezaji wa Mwongozo huu.
iv. Kufuatilia zoezi la uuzaji na ununuzi wa korosho ghafi kutoka kwenye Soko la Awali.
v. Kuhakikisha kila mnunuzi amelipa wakulima na tozo zote zilizoanishwa katika Mwongozo huu.

vi. Kusimamia utekelezaji wa Mwongozo huu ndani ya Halmashauri husika.

**4.7. Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania**

i. Kusimamia UNION na AMCOS ili kuhakikisha kuwa wanatekeleza majukumu yao kwa kuzingatia mwongozo huu.

ii. Kuchukua hatua za kisheria kwa vyama vya ushirika vitakavyobainika kukiuka taratibu za utekelezaji wa Soko la Awali kwa mujibu wa Mwongozo huu.

iii. Kusimamia utekelezaji wa Mwongozo huu ndani.

**4.8. Chama Kikuu cha Ushirika (*Union*)**

i. Kuratibu utekelezaji wa Soko la Awali katika eneo husika,

ii. Kufuatilia mwenendo wa ununuzi wa korosho ghafi kupitia Soko la Awali ndani ya eneo husika.

iii. UNION kusaidia upatikanaji wa korosho ghafi kwa wabanguaji wa ndani kwa kuwapa taarifa ya uwepo wa korosho katika maeneo yao.

iv. Kutoa taarifa Halmashauri kuhusiana na malipo ya korosho zilizonunuliwa ili kuiwezesha halmashauri kutoa idhini ya kusafirisha korosho hizo.

**4.9. Chama cha Ushirika cha Msingi (AMCOS)**

i. Kuratibu kikao cha mapatano/makubaliano ya bei kati ya Mkulima na Mbanguaji anaehitaji kununua korosho katika Soko la Awali

ii. Kuandaa muhtasari wa makubaliano ya kuuza korosho na kuhifadhi orodha ya majina ya wakulima waliouza korosho kupitia soko la awali katika AMCOS husika,

iii. Kusimamia malipo ya korosho kwa kuzingatia bei itakayokubaliwa na wakulima katika Soko la Awali.

iv. Kuhakikisha kuwa korosho zitakazouzwa na wakulima katika Soko la Awali zinakidhi viwango vya ubora kwa kuzingatia Mwongozo wa Usimamizi na udhibiti Ubora wa Korosho wa mwaka 2025/2026.

v. Kuhakikisha malipo kwa wakulima wanaouza korosho ghafi katika Soko la

Awali yanafanyika ndani ya siku 2 baada ya makubaliano na mkulima kulipwa fedha kupitia benki.

vi. Kutoa taarifa kwa Halmashauri na Chama Kikuu kuhusiana na malipo ya korosho zilizonunuliwa ili kuiwezesha halmashauri kutoa idhini cha kusafirisha korosho hizo.

vii. Kuainisha majina na akaunti za wakulima watakaouza korosho zao kwa mbanguaji kwa ajili ya malipo.

viii. Kutoa taarifa kwa wakati kwa Mamlaka za usimamizi juu ya ukiukwaji wowote wa taratibu za Soko la Awali kwa mujibu wa Mwongozo huu.

### 4.10. Mbanguaji wa Ndani

i. Kusaini mkataba wa ununuzi wa korosho ghafi katika soko la awali kwa msimu2025/2026.

ii. Kuomba leseni ya ubanguaji wa korosho nchini.

iii. Kujisajili katika Umoja wa Wabanguaji (TACP).

iv. Kuomba leseni ya ununuzi wa korosho ghafi katika Soko la Awali kupitia mfumo wa wizara ya kilimo (e-kilimo).

v. Kubangua korosho zote atakazonunua kutoka kwenye Soko la Awali.

vi. Kulingana na hali ya soko ilivyo wabanguaji watajadiliana na wakulima kupata bei.

vii. Kutunza kumbukumbu za malipo aliyoyafanya kwa korosho alizonunua kutokakwenye AMCOS husika.

### 4.11. Umoja wa Wabanguaji wa Korosho nchini TACP

i. Kusimamia na kuhakikisha kwamba korosho zinazonunuliwa kupitia Soko la Awali zinabanguliwa hapa nchini.

ii. Kusajili wabanguaji wa korosho ghafi.

iii. Kutoa taarifa ya mwenendo wa ubanguaji wa korosho nchini kila mwezi kwa Bodi ya Korosho.

iv. Kutoa taarifa kwa Timu ya usimamizi juu ya changamoto zozote zinazojitokeza katika utekelezaji wa mwongozo huu na mapendekezo ya namna ya kuzitatua changamoto hizo.

v. Kutoa taarifa kwa mamlaka husika pale inapotokea ukiukwaji wowote wa taratibu miongoni mwa wanachama.

vi. Kuimarisha ushirikiano baina ya wabanguaji na wadau mbalimbali katika Tasnia ya Korosho kama vile Vyama vya Msingi (AMCOS), Vyama Vikuu vya Ushirika, Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGAs) , na Bodi ya Korosho Tanzania (CBT).

vii. Kutoa Elimu ya Umuhimu wa Soko la Awali kwa wadau.

### 4.12. Mkulima wa Korosho

i. Ana hiari ya kuuza korosho ghafi kwenye Soko la Awali au soko la upili

ii. Kuhakikisha anapeleka korosho zenye viwango vya bora vinavyokubalika nchini na kuhifadhiwa katika magunia

iii. Kuvuna korosho na kupanga katika madaraja kabla ya kupeleka katika AMCOS kwa ajili ya uuzaji kwa Mbanguaji.

iv. Kushiriki kikao cha kukubaliana bei ya kuuzia korosho na Mbanguaji husika katika soko la Awali.

v. Kuwa na akaunti benki kwa ajili ya kupokelea malipo ya korosho.

vi. Kuepuka kuchanganya korosho na vitu visivyo korosho ikiwa ni pamoja na korosho zilizoharibika.

vii. Kuzingatia gharama za uzalishaji wa korosho wakati wa mapatano ya bei ya kuuzia korosho kwa Mbanguaji ili kukubaliana bei inayompatia faida.

viii. Kutoa taarifa kwa mamlaka husika pale inapotokea ukiukwaji wowote wa taratibu za Mwongozo huu.

### 4.13. Taasisi za Fedha

i. Kutoa huduma za fedha kwa wakulima na wabanguaji ili waweze kufikia malengo.

ii. Kuhakikisha malipo ya wakulima yanafanyika kwa wakulima ndani ya saa 24

iii. Kuhamasisha wakulima na wabanguaji kutumia huduma za kibenki.

iv. Kuwatembelea na kuwafungulia akaunti wakulima kwa ajili ya kupokelea malipo yakorosho.

v. Kutoa uthibitisho wa uwezo wa mbanguaji kufanya malipo ya korosho

atakazonunua katika soko la Awali pale itakapohitajika.

## 5.0 MAKOSA NA ADHABU

i. **Kununua korosho kwenye Soko la Awali bila kibali.** Korosho husika zitataifishwa kwa mujibu wa Sheria ya Tasnia ya Korosho Na. 18 ya Mwaka 2009 na Kanuni za Mwaka 2010.

ii. **Kuchelewa kufanya malipo kwa Mkulima** ndani ya siku mbili (2) baada ya kukamilika taratibu za mauziano na iwapo mnunuzi atashindwa kulipa atatozwa faini ya asilimia 5% ya thamani ya mzigo aliyonunua.Mkulima kupitia AMCOS husika anaruhusiwa kuuza kwa mbanguaji mwingine au Soko la Upili (Mnada).

iii. **Kusafirisha korosho ghafi zilizonunuliwa kwenye Soko la Awali kwenda masoko ya nje ya nchi.** Korosho husika zitataifishwa na Bodi ya Korosho ikiwa ni pamoja na kusitisha Leseni ya ununuzi wa korosho ghafi kutoka Soko la Awali iliyotolewa kwa mbanguaji husika.

## 6.0 USULUHISHI WA MIGOGORO

i. Endapo kutatokea malalamiko/mgogoro kati ya wadau kwenye tasnia ya korosho, kwa kutegemeana na aina ya malalamiko/mgogoro husika, malalamiko yapelekwe Bodi ya Korosho kwa utatuzi.

ii. Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Korosho Tanzania anaweza kuunda Timu Maalum ya kusimamia utekelezaji wa Soko la awali na kutatua changamoto yoyote katika soko la awali na kutoa mapendekezo.

iii. Endapo malalamiko/migogoro hiyo haitakuwa imetatuliwa na Bodi ya Korosho Tanzania, mamlaka zingine husika zitahusishwa.

## 7.0 HITIMISHO

Mwongozo huu unasomwa sambamba na Sheria ya Tasnia ya Korosho Na. 18 ya Mwaka 2009, Kanuni zake za Mwaka 2010 pamoja na Miongozo mingine inayotolewa na Bodi ya Korosho Tanzania. Aidha, utekelezaji wa Mwongozo huu unazingatia sheria zingine za nchi zinazosimamiwa na taasisi zingine za serikali zinazohusika katika tasnia ya korosho kwa kuzingatia mnyororo wa thamani. Hata hivyo Mwongozo huu ukitekelezwa kama ulivyokusudiwa utaongeza kasi ya ubanguaji na kusaidia ukuaji wa viwanda vya ndani kwa kuwezesha viwanda vya ndani kupata malighafi kwa urahisi na kwa wakati. Vile vile kuongeza ajira na kukuza pato la taifa.

Mwongozo huu umetolewa leo tarehe 28 Agosti Mwaka 2025.

Francis Alfred

**MKURUGENZI MKUU.**